

# RC aagiza kutungwa sheria ndogo wanaopitisha mifugo barabarani

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, ameziagiza halmashauri za mkoa huo kuboresha sheria ndogo ili kuwabana wafugaji wanaopitisha mifugo yao katika barabara na kuigharimu serikali kutumia fedha nyingi kufanya matengenezo.

Queen alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao cha Bodi ya Barabara alipozungumza na wajumbe wa Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Manyara.

"Halmashauri nendeni mboreshe sheria ndogo na kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya barabara ili tuokoe barabara zetu maana tunatumia fedha nyingi kuzifanyia matengenezo," alisema Sendiga.

Alisema wakurugenzi na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) wakianza kusimamia sheria ndogo na viongozi wa kisiasa wanyamaze wasiwatetee wafugaji.

"Wanasiasa tuache kupiga simu kwa mabosi wangu, niambieni mimi wakati mwingine mnanipa hofu," alisema.

Kuhusu ahadi za viongozi, Mkuu wa Mkoa aliagiza sekta zote zipeleke mpango kazi ofisini kwake kuonesha namna ya kwenda kutekeleza ahadi hizo.

"Ni lazima ahadi za viongozi zitekelezwe na madaraja makongwe ni vizuri kuyaangalia namna ya kuyatengeneza," alielekeza.

Awali Kaimu Meneja wa TANROADS mkoani Manyara, Dutu Masele, akiwasilisha taarifa yake, alisema wameishafanya uthamini kwa wananchi wanaotakiwa kulipwa fidia itakapopita barabara ya mchepuko ambapo Sh. bilioni tisa zitatolewa kuwalipa.

"Tumeishawasilisha wizarani ombi la kulipa fidia barabara ya mchepuko ya kilometa 25," alisema Masele.

Meneja huyo alitaja vikwazo ambavyo wanakabiliana navyo kuwa ni pamoja na mfumo wa ununuzi kuchelewa, mifugo kutembezwa barabarani, ufinyu wa bajeti na kutupa taka kwenye mitaro.

Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alisema kama hawatawapa kazi makandarasi wazawa hawatainuka kiuchumi badala yake makandarasi wa kigeni ndio wataendelea kunufaika.

Queen aliitaka TANROADS kushirikisha wabunge kwenye kazi wanazofanya kabla hawajaanza.

Kaimu Meneja wa TARURA Mkoa wa Manyara, Edwin Magiri, akitoa taarifa yake alisema utekelezaji miradi ya maendeleo umefikia asilimia 65 na mikataba 74 ya ujenzi wa barabara imeishatiwa saini.